

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BUNGE LA TANZANIA**



**MKUTANO WA TATU**

**YATOKANAYO NA KIKAO CHA KUMI**

**2 MEI, 2016**

**MKUTANO WA TATU**  
**YATOKANAYO NA KIKAO CHA KUMI - TAREHE 2 MEI, 2016**

**I. DUA**

Saa 3.00 asubuhi Mhe. Dkt. Tulia Ackson (NAIBU SPIKA) alisoma Dua na kuliongoza Bunge.

**Makatibu Mezani**

1. Ndg. Neema Msangi
2. Ndg. Joshua Chamwela

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani.

1. Mhe. Mwigulu Lameck Nchemba aliwasilisha Mezani Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;
2. Mhe. Luhaga Joelson Mpina aliwasilisha Mezani Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;
3. Mhe. Mohammed Omary Mchengerwa aliwasilisha Mezani Taarifa ya Kamati ya Katiba na Sheria kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;
4. Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu aliwasilisha mezani Taarifa ya Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;
5. Mhe. Pauline Philipo Gekul aliwasilisha mezani taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;
6. Mhe. Pauline Philipo Gekul aliwasilisha Mezani Taarifa ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

### **III. MASWALI:**

Maswali yafuatayo yaliulizwa:-

#### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

Swali Na.72 – Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu

Swali la nyongeza: Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu

Swali Na.73 – Mhe. Kemilembe Julius Lwota

Swali la nyongeza: Mhe. Kemilembe Julius Lwota

#### **WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

Swali Na.74 – Mhe. Amina Nassoro Makilagi

Swali la nyongeza: (i) Mhe. Amina Nassoro Makilagi

(ii) Mhe. John Peter Kadutu

#### **WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

Swali Na.75 – Mhe. Marwa Ryoba Chacha

Swali la nyongeza: Mhe. Marwa Ryoba Chacha

#### **WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Swali Na.76 – Mhe. Esther Nicholas Matiko

Swali la nyongeza: Mhe. Esther Nicholas Matiko

#### **WIZARA YA NISHATI NA MADINI:**

Swali Na.77 – Mhe. Dunstan Luka Kitandula [kny Mhe. Mary Pius Chatanda]

Swali la nyongeza: Mhe. Mary Pius Chatanda

Mhe. Dunstan Luka Kitandula

Swali Na.78 – Mhe. Hassan Elias Masala

Swali la nyongeza: (i) Mhe. Hassan Elias Masala

#### **WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

Swali Na.79 – Mhe. Rashid Ali Abdallah

Swali la nyongeza: Mhe. Rashid Ali Abdallah

Swali Na.80 – Mhe. Maria Ndila Kangoye

Swali la nyongeza: (i) Mhe. Maria Ndila Kangoye

(ii) Mhe. Ritta Enespher Kabati

#### **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Swali Na.81 – Mhe. Ally Keissy Mohammed

Swali la nyongeza: Mhe. Ally Keissy Mohammed

Swali Na.82 – Mhe. Eng. Atashasta Justus Nditiye

Swali la nyongeza: Mhe. Eng. Atashasta Justus Nditiye

#### **IV. MATANGAZO:**

##### **WAGENI:**

- Wageni 21 wa Mhe. January Yussuf Makamba ambao ni viongozi wa Ofisi yake na wageni wake wengine.
- Wageni 8 wa Mhe. Angeline Silvester Mabula.
- Wageni 4 wa Mhe. Zacharia Paulo Issaay ambao ni Madiwani wa Mji wa Mbulu.
- Mgeni wa Mhe. Mohammed Omary Mchengerwa.
- Wageni 18 wa Mhe. Margareth Simwanza Sitta kutoka TWPG.
- Wanachuo 145 na Walimu 5 kutoka Chuo cha Zioni – DSM.

#### **V. KAZI:**

- (i) Wabunge wanakumbushwa kujisajili kupitia utaratibu mpya wa *Biometric*.
- (ii) Wabunge wanawake wanaalikwa kwenye tafrija leo saa 2.00 usiku itakayofanyika katika Ukumbi wa St. Gaspar.

#### **VI. UAMUZI WA SPIKA KUHUSU MIONGOZO YA WABUNGE:**

- Mhe. Naibu Spika alitoa uamuzi wake kuhusu miongozo iliyoombwa na Wabunge wafuatao:-
  - i) Mhe. Dkt. Immaculate Sware Semesi.
  - ii) Mhe. Zainab Matitu Vullu.
  - iii) Mhe. Mwita Mwikwabe Waitara.

#### **MIONGOZO:**

1. Mhe. Devotha Mathew Minja alisimama kuomba mwongozo chini ya Kanuni ya 68(7) na 46(1) kwamba swali la pili la nyongeza la Mhe. Marwa Ryoba Chacha halikujibiwa kabisa na Serikali.

Naibu Spika alieleza kuwa Kanuni ya 46(1) inahusu hasa majibu ya Swali la msingi na siyo la nyongeza, malalamiko kuhusu swali la nyongeza yaletwe ili kiti kifuatilie na kutoa maelezo.

2. Mhe. Mohammed Ally Keissy aliomba mwongozo chini ya Kanuni ya 46(1) kwamba Swali lake halikujibiwa vizuri na Naibu Waziri Eng. Stella Manyanya pamoja na uelewa wake mkubwa wa Wilaya ya Nkasi.

Naibu Spika alieleza kuwa ameshalitolea maelezo suala hilo.

3. Mhe. Marwa Ryoba Chacha aliomba mwongozo chini ya Kanuni ya 68(7) kwamba Naibu Spika amekuwa akimuonea kila mara anapouliza swali, aliomba kujua ana shida gani.

Mhe. Naibu Spika alieleza kuwa ni Mbunge mwenyewe ambaye amekuwa akitoa lugha zisizofaa dhidi ya kiti na pia leo ametoa maelezo marefu sana ya ziada badala ya kuuliza swali na ni wajibu wa kiti kuwakumbusha Wabunge kuhusu kuzingatia Kanuni:

#### **VII. HOJA ZA SERIKALI:**

- Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Januari Yussuf Makamba alisoma Hotuba ya Bajeti ya Ofisi hiyo na kutoa Hoja ya kuliomba Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;
- Mhe. Mohammed Omary Mchengerwa alisoma Taarifa ya Kamati ya Katiba na Sheria kuhusu Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;
- Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu alisoma Taarifa ya Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;
- Mhe. Ally Saleh Ally alisoma Taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;
- Mhe. Pauline Gekul alisoma Taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

#### **MATANGAZO:**

- Mahudhurio ya *biometric* ni mara 2 kwa siku kwenye vituo vya ukumbi huu.
- Matokeo ya mechi dhidi ya Wabunge na Watumishi yalisomwa.

#### **VIII. KUSITISHA BUNGE:**

Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 10.00 jioni.

## **IX. BUNGE KUREJEA:**

- Saa 10.00 Jioni Bunge lilirejea na kuongozwa na Mwenyekiti, Mhe. Andrew John Chenge.

Hoja ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira iliendelea na Wabunge wafuatao walipata nafasi ya kuchangia:-

1. Mhe. Dkt. Immaculate Siware Semesi	-	CHADEMA
2. Mhe. Dotto Gimbi Masaba	-	CHADEMA
3. Mhe. Khatib Said Haji	-	CUF
4. Mhe. Hafidh Ali Tahir	-	CCM
5. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	-	CCM
6. Mhe. Fakharia Shomar Khamis	-	CCM
7. Mhe. Silafu Jumbe Maufi	-	CCM
8. Mhe. Faida Mohammed Bakar	-	CCM
9. Mhe. Salum Mwinyi Rohani	-	CCM
10. Mhe. Khamis Mtumwa Ali	-	CCM
11. Mhe. Khadija Hassan Aboud	-	CCM
12. Mhe. Ali Hassan Omar King	-	CCM
13. Mhe. Hamad Yussuf Masauni (NW)	-	CCM
14. Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi (W)	-	CCM
15. Mhe. George Mcheche Masaju	-	AG

## **X. KUHITIMISHA HOJA:**

Uhitimishaji wa Hoja ulianza kwa Naibu Waziri Mhe. Luhaga Joelson Mpina kujibu Hoja za Wabunge na kufuatiwa na Mtoa Hoja, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na mazingira) Mhe. Januari Yussuf Makamba.

## **XI. KAMATI YA MATUMIZI:**

Baada ya uhitimishwaji Bunge liliingia katika hatua ya Kamati ya Matumizi, na kuanza na Fungu 26 (Makamu wa Rais), wafuatao walichangia:-

1. Mhe. Masoud Abdallah Salim – CUF

**Fungu 31 (Ofisi ya Makamu wa Rais) Wabunge wafuatao walichangia:-**

2. Mhe. Kasuku Samson Bilago (CHADEMA) alitoa shilingi na wafuatao walichangia:-
  - i) Mhe. Susan Limbweni Kiwanga

- ii) Mhe. Hamidu Hassan Bobali
- iii) Mhe Daniel Nicodemus Nsanzugwanko
- iv) Mhe. John Wegesa Heche
- v) Mhe. Jitu Vrajlal Soni
- vi) Mhe. Albert Obama Ntabaliba
- vii) Mhe. Hussein Mohamed Bashe
- viii) Mhe. Dkt. Hamis Andrea Kigwangala
- ix) Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia
- x) Mhe Selemani Said Jafo
- xi) Mhe. Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo
- xii) Mhe. Charles Muhangwa Kitwanga
- xiii) Mhe. Jenista Joakim Mhagama

- 3. Mhe. Masoud Abdallah Salim
- 4. Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa
- 5. Mhe. Jitu Vrajlal Soni
- 6. Mhe. Maida Hamad Abdallah

**TAARIFA:**

Bunge lilipitisha mafungu yote ya Ofisi hiyo bila Mabadiliko yoyote, Hoja ilitolewa na kuungwa mkono, Wabunge walihojiwa na kupitisha Bajeti husika.

**TANGAZO:**

Wabunge wanawake mnakaribishwa St. Gaspar kwenye hafla.

**MWONGOZO:**

Mhe. Pauline Philipo Gekul aliomba mwongozo kupitia Kanuni ya 68(7) na kuuliza kwa nini Serikali haijaleta kitabu cha Volume I.

Mwenyekiti aliahidi kulifanyia kazi kwa kushirikiana na Serikali na jibu litatolewa.

**XII. KUAHIRISHA SHUGHULI ZA BUNGE**

Saa 2:30 Usiku Mhe. Mwenyekiti aliahirisha Bunge hadi tarehe 3/5/2016 siku ya Jumanne saa 3.00 asubuhi.

**DODOMA  
2 MEI, 2015**

**DKT. T. D. KASHILILAH  
KATIBU WA BUNGE**